



وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنْكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لِيَسْتَخْلِفُوهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا أَسْتَخْلَفَ
الَّذِينَ مِنْ قَبْلِهِمْ وَلَيُكَذِّبَنَّهُمْ وَيُنَاهِيَ اللَّهُ أَرْجُونَهُمْ وَلَيُكَذِّبَنَّهُمْ مَنْ بَعْدَ حَقِيقَتِهِمْ أَمَّا
يَعْبُدُونَ فَلَا يُشْرِكُونَ بِإِلَهٍ وَمَنْ كَفَرَ بَعْدَ ذَلِكَ فَأُولَئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ

Toleo: 1441 / 03

Jumatatu, 22 Dhu al-Qa'adah 1441 H

13/07/2020 M

Taarifa Kwa Vyombo vyta Habari

TUNASIMAMA IMARA NA FAMILIA NA MAHABUSU

Kufuatia mkutano wa waandishi habari wa wawakilishi wa familia tatu za mahabusu: Omar Salum Bumbo, Ramadhan Moshi Kakoso, na Waziri Suleiman Mkaliaganda mnamo 09 Julai 2020 huko Magomeni Makuti, Dar es Salaam, Tanzania ili kuelezea huzuni na uchungu wao juu ya jamaa zao watatu ambao wanazuiliwa pasi na mashtaka kwa takriban miaka mitatu, sisi katika Hizb ut Tahrir / Tanzania tunasimama imara kwa mshikamano na familia hizi (za mahabusu) ambao ni wanachama wa Hizb ut Tahrir / Tanzania ili kudai haki kwao.

Sisi katika Hizb ut Tahrir / Tanzania kwa mara nyengine tena tunavitaka vyombo vyote vinavyo husika na utoaji haki nchini Tanzania kuzingatia mchakato sahihi wa mahakama kwa kufikisha ushahidi mahakamani tayari kwa mashtaka ya mahabusu, endapo watakuwa na ushahidi wowote, waachilieni mahabusu hao watatu kwa dhamana, au waachilieni huru mara moja.

Masoud Msellem

Mwakilishi kwa Vyombo vyta Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania

Alama Ishara

#StopOppressiveLawsAndAbduction (Kiingereza)

#KomeshuUkandamizajiWaKisheriaNaUtekaji (Swahili)